# Kabla ya Chekechea / Wahudumu wa Maandalizi wa Chekechea - 1/2

Mtoto wako anapokaribia umri wa kuenda shule kwa kasi, huenda unashindwa kama mtoto wako amepata ujuzi unahitajika kufaulu katika sehemu hii mpya na yenye changamoto ya utotoni mwake. Ili kumsaidia mtoto wako katika mpito huu, Mpango wa Elimu ya Wahamiaji Pennsylvania (Pennsylvania Migrant Education Program) umekupa orodha ifuatayo ya tabia zinazoangaliwa kila wakati na wilaya za shule na mipango ya kabla ya shule ili kubaini kama mtoto wako anaweza kupata ujuzi wa shule unaohitajika anapopitia shule. Kushirikiana na mtoto wako nyumbani kutasaidia kuhakikisha mpito laini na wenye raha hadi ndani ya shule. Tafadhali kumbuka: mtoto yeyote anayetimiza umri unahitajika kujiunga na chekechea anastahiki kuhudhuria chekechea. Rasilimali hii haipaswi kuwahi kutumika kumtenga mtoto yeyote aliyehitimu umri kutojiunga na chekechea.

| Ndiyo | Bado | # | Ukuaji wa Kijamii na Kihisia | Mfano wa Ndiyo |
|---|---|---|---|---|
| | | 1 | Mtoto wako anakabiliana vipi na hali ya kutenganishwa na mama na baba? | Mtoto anatenganishwa kwa urahisi na kwa furaha. |
| | | 2 | Mtoto wako anajua jina la kila mtu anayeishi nyumbani? | Mtoto anawatambua watu wote kwa jina na anasema kitu anachojua kumhusu kila mtu. |
| | | 3 | Mtoto wako anasuluhisha migogoro rahisi pekee yake? | Mtoto anasuluhisha migogoro pekee yake, huku akifikiri kuhusu mahitaji na matamanio yake na ya wengine. |
| | | 4 | Mtoto wako anaelewa sheria na madhara? | Mtoto anajua na kufuata sheria na anaweza kuelezea sababu ya kuwepo kwa sheria hizi. |

| Ndiyo | Bado | # | Ukuaji wa Lugha na Kusoma/Kuandika | Mfano wa Ndiyo |
|---|---|---|---|---|
| | | 1 | Mtoto wako anajua jina lake kamili na umri wake? | Mtoto anataja jina lake kamili na anatumia vidole kuonyesha umri wake. |
| | | 2 | Mtoto wako anaweza kutofautisha kati ya herufi na nambari? | Mtoto anatambua na kutaja baadhi ya herufi na baadhi ya nambari. |
| | | 3 | Mtoto wako anaweza kutambua upande wa mbele, upande wa nyumba na jina la kitabu? | Mtoto anaweza kutambua vipengee vyote tatu. |
| | | 4 | Mtoto wako anaweza kusimulia mtiririko sahihi wa hadithi? | Mtoto anaweza kusimulia hadithi kuhusu picha au matukio katika mpangilio sahihi. |
| | | 5 | Mtoto wako anaweza kuandika jina akitumia michoro inayofanana na herufi au herufi za kawaida? | Mtoto anaweza kuandika jina lake la kwanza pekee yake, huku herufi nyingi zikiwa sahihi. |
| | | 6 | Mtoto wako anafuatiliza hatua anapopewa maelekezo ya hatua mbili? | Mtoto anafuata maelekezo na anaelewa kusudi. |
| | | 7 | Mtoto wako anashiriki hisia anapoulizwa? | Mtoto anazungumzia mawazo, hisia na dhana zake binafsi. |
| | | 8 | Mtoto wako anazungumza kwa sentensi kamili? | Mtoto anaweza kuwasiliana kwa Kiingereza akitumia sentensi kamili. |

| Ndiyo | Bado | # | Kufikiri Kihisabati na Kujieleza | Mfano wa Ndiyo |
|---|---|---|---|---|
| | | 1 | Mtoto wako anaweza kuhesabu kuanzia 1 hadi angalau 20? | Mtoto anahesabu kuanzia 1 hadi 20. |
| | | 2 | Mtoto wako anaweza kutambua angalau maumbo 4 (mfano: Mraba,duara, pembe tatu, mstatiri) | Mtoto anatambua na kutaja maumbo 4. |
| | | 3 | Mtoto wako anaweza kuelezea eneo la vitu vya kila siku? | Mtoto anatumia maneno ya maeneo (kwenye, nyuma, chini, karibu, mbele, n.k) au maneno ya mpangilio (kwanza mwisho, n.k) ili kuelezea eneo la kitu. |
| | | 4 | Mtoto wako anaweza kuainisha, kulinganisha, kupanga kwa makundi angalau vitu 5 kulingana na vipengele vyake kama vile ukubwa, wingi, umbo au rangi? | Mtoto anaainisha vitu kwa kutumia kipengele kimoja. Mtoto alitenganisha wanyama na magari. |

# Kabla ya Chekechea / Wahudumu wa Maandalizi wa Chekechea - 2/2

| Ndiyo | Bado | # | Mikabala kwa Mafunzo kupitia Michezo | Mfano wa Ndiyo |
|---|---|---|---|---|
| | | 1 | Mtoto wako anafurahia mada, dhana na shughuli mpya? | Mtoto anauliza maswali ili kuelewa jambo jipya. Mtoto anataka kujifunza mambo mapya. |
| | | 2 | Mtoto wako anasikiliza na kuchangamkia hadithi au shughuli inayochukua zaidi ya dakika 15? | Mtoto anaweza kusalia kwenye shughuli hata wakati shughuli hiyo inapokuwa na changamoto. |
| | | 3 | Mtoto anatumia fikira zake na ubunifu wake kucheza na vitu? | Mtoto anaweza kucheza akitumia vitu tofauti kwa kuvipea vitendo na mwenendo. |
| | | 4 | Mtoto wako anaweza kusuluhisha matatizo akiwa pekee yake? | Mtoto anajaribu kusuluhisha matatizo kwa zaidi ya njia moja. |

| Ndiyo | Bado | # | Afya, Uzima, na Ukuaji Kimwili | Mfano wa Ndiyo |
|---|---|---|---|---|
| | | 1 | Mtoto wako anaweza kutambua na kuonyesha sehemu za mwili? | Mtoto anaweza kutambua na kutaja jina la sehemu kadhaa za mwili bila usaidizi wowote. |
| | | 2 | Mtoto wako anaweza kutekeleza mtindo rahisi akiwa pekee yake? | Mtoto amefunzwa kuenda msalani<br>Mtoto anaweza kuosha mikono,<br>Mtoto anajivisha nguo,<br>Mtoto anapiga mswaki,<br>Mtoto ana mtindo wa saa za kulala. |
| | | 3 | Mtoto wako anaweza kula na kunywa akiwa pekee yake akitumia vyombo vinavyofaa? | Mtoto anatumia uma, kijiko, kisu, kitambaa, sahani, bakuli na kikombe kwa njia mwafaka. |
| | | 4 | Mtoto wako anaonyesha ushirikiano katika kutembeza mwili wakati wa mchezo amilifu au unaohusisha kutembeza viungo vya mwili? | Mtoto anaweza kutembea juu na chini ya gorofa. Mtoto anaweza kukimbia na kugonga mpira kwa mguu. |
| | | 5 | Mtoto wako anaweza kuvaa na kuvua mavazi za juu (koti, viatu, kofia, glavu) na akiwa pekee yake? (pamoja na kufunga zipu, vifungo, na kufunga kamba). | Mtoto anaweza kuvaa na kuvua mavazi akiwa pekee yake; soksi, viatu, suruali, shati, koti, glavu na kofia. |
| | | 6 | Mtoto anaweza kutumia makasi kwa udhibiti na kusudi? | Mtoto anakata kwa mstari sambamba na kwa vizingo. |
| | | 7 | Mtoto wako anaweza kuandika na kuchora akiwa ameshika kalamu vizuri. | Mtoto anatumia vidole tano, nne au tatu kushika kalamu anayoandikia. |

Mtoto wangu ana NDIYO _____________.